

Watumishi wa Tume watakiwa Kuzingatia Maadili ya utumishi wa Umma

Watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wametakiwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa umma kwani wao ni kioo katika jamii na wanapaswa kuwa mfano kwa taasisi nyingine na kwa jamii kwa ujumla kwani taasisi yao ni muhimili muhimu wa kukuza Demokrasia nchini.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi Kailima Ramadhan ijumaa tarehe 24-6-2016 alipokutana na Watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao maalumu cha Kutekeleza maagizo ya Katibu Mkuu kiongozi aliozitaka Taasisi za Serikali kutumia Wiki ya Utumishi wa Umma kusikiliza Kero za watumishi pamoja na kusikiliza Kero za Wananchi.

Pia amewataka watumishi hao kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha malengo ya Taasisi wakati huu ambao Tume inaanza kipindi kingine cha mzunguko wa Uchaguzi kufuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa 2015 kulikohitimishwa na Taarifa ya Uchaguzi iliyokabidhiwa kwa Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli.